


KUMBUKIZI YA 1 MZEE HAMISI AKIDA



MZEE HAMISI AKIDA

UMEKATIKA MKUFU: HAMISI AKIDA NA ZACHARIA MOCHIWA

*Saidi A. Ngatuma
(Bahari ya Hekima)*

Mependa wetu raufu, ewe Mola msifika,
Usiye na upungufu, usiye na mshirika,
Twaomba dua sufufu, mbele yako twaanguka,
Sote tunawakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.

Umekatika mkufu, hauwezi kuungika,
Chapachapa hamchifu, machozi yatumwagika,
Simanzi na nyangi hofu, mihimili imeng'oka,
Sote tunawakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.

Dunia twaiarifu, wenzenu tumeumbuka,
Mabingwa wa usanifu, dunia wametutoka,
Tulipo tumedhoofu, hatuna la kulishika,
Sote tunawakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.

Watu hawa ashrafu, majina nawaandika,
Akida muadilifu, bingwa wa kuaminika,
Alikuwa maarufu, hata nje ya mipaka,
Sote tunawakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.

Akida ametawafu, bado anahitajika,
Ndiye yeye mbunifu, hamiroja kusomeka,
Katwacha wanyong'onyefu, wakiwa twasononeka,
Sote tunawakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.

Mwalimu mbanifu, Mochiwa alosifika,
Alipenda unyoofu, wa lugha kutamikika,
Hakika katika safu, mabingwa wamepunguka,
Sote tunawakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.

Mochiwa tulimsifu, kwa kutokughadhibika,
Jambo likimkalifu, yeye daima hucheka,
Kwayo yaliyomkifu, papara aliepuka,
Sote tunawakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.

Walikuwa na insafu katika kuwajibika,
Walijitoa wakfu, muda wote kutumika,
Wajawa na masharifu, tuwaombee baraka,
Sote tuna wakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.

Hakuna wa kuhalifu, amri yako Rabuka,
Tunaomba tahafifu, wape nuru ya kuwaka,
Waweke patakatifu, peponi kupumzika,
Sote tunawakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.

Tamati mwendo mrefu, hauhitaji haraka,
Hakuna mkamilifu, asoweza kupotoka,
Ni kubwa wao wakifu, usoweza kupimika,
Sote tuna wakumbuka, mabingwa wa Kiswahili.